

Bibilia ya watoto
Inaleta

Kuzaliwa
kwake Yesu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: M. Maillot;
Alastair Paterson

Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii,
lakini bila ya kuuza.



Hapo zamani,
Mungu alimtuma
malaika Gabrieli kwa
mwanamali mdogo

n a wa
kupendeza
aliyeitwa
Maria.



Akamwambia, "Wewe utazaa
mwana na jina lake utamuita
Yesu. Yeye ataitwa
mwana wa aliye juu.

Yeye
atamiliki
milele."



"Hii itakuaje?" binti
Yule aliuliza akiwa
ameshangaa. "Mimi
sijaolewa na
mwanamume
yeyote."



Malaika akamwambia
Maria kuwa mtoto
angetoka kwa Mungu.
Mtoto Yule
hangekuwa
na baba wa
kibinadamu.



Malaika pia akamwelezea
Maria kuwa jamaa
yake Elisabeti
alikuwa
amepata
mimba katika
uzee wake.



Maria alikuwa
amepanga kuolewa
na Yusufu.

Yusufu
alisikia
vibaya
aliposikia
kuwa Maria
alikuwa
mjamzito.



Alidhania kuwa
mwanamume
mwingine
alikuwa ndiye
baba ya
mtoto.



Katika ndoto, malaika wa Mungu alimwambia Yusufu ya kuwa huyu alikuwa mwana wa Mungu. Naye Yusufu alikuwa amsaidie Maria kumlelea Yesu.



Yusufu alimwamini na kumtii Mungu.
Naye pia alitii
amri za nchi
yake.



Kwasababu ya amri moja, Yusufu na
Maria walisafiri
kutoka
kwao hadi



Bethlehemu,
ili kulipa ushuru.



Maria alikuwa
tayari kumzaa
mtoto.



Lakini Yusufu
hakuweza
kupata nyumba
ya kukaa.



Nyumba
zote zilikuwa
zimejaa.



Mwishowe Yusufu aliweza kupata
malazi horini. Hapo,
mtoto Yesu
akazaliwa.



Mama yake akamlaza ndani ya hori
la kulia la ng'ombe.



Karibu na hapo, wachungaji walikuwa
wakiwachunga kondoo

wao.



Malaika wa Mungu akawatokea na kuwapa habari lile njema.



"Amezaliwa kwenu siku ya leo katika
mji wa Daudi mwokozi,
ndiye Kristo
Bwana.



Mtamkuta mtoto amelala katika hori ya kulia ya ng'ombe."



Ghafila, malaika wengi wengine
wanaong'aa wakatokea,
wakimsifu



Mungu
wakisema, ...



... "Atukuzwe Mungu juu mbinguni,
na duniani iwe amani
kwa watu



aliowaridhia."



Wachungaji wakaharakisha
kuelekea horini.



Baada ya kumwona
mtoto walimweleza kila
waliokutana nao kumhusu
Yesu.





Muda wa siku
arobaini
baadaye,
Yusufu
na Maria
walimleta
Yesu kwenye
hekalu kule
Yerusalemu.





Hapo, mwanamume
aliyeitwa Simioni
alimtukuza
Mungu kwa
sababu ya
mtoto, ...





... naye Anna,
mtumishi
mwingine
wa Mungu,
akamshukuru
Mungu.





Wote walifahamu
kuwa Yesu alikuwa
mwana wa
Mungu,
mwokozi
aliyekuwa
ameahidiwa.



Yusufu akawatoa
ndege wawili
kama sadaka.





Hii ilikuwa sadaka
ambayo kulingana
na amri ya
Mungu watu
masikini ...





... walipaswa
kuleta
walipokuwa
wanamletea
Mungu
mtoto
aliyezaliwa.



Muda mfupi ulipopita,
nyota ya kipekee
iliwaongoza
wazee

watatu wenye
hekima kutoka nchi
ya Magharibi kuja
Yerusalemu.



"Yuko wapi
Mfalme wa
Wayahudi
aliyezaliwa?"

wakauliza.
"Tunataka
kumwuabudu."



Mfalme
Herodi
akasia
kuwahusu wale
wazee wenye
hekima.



Akiwa na
wasiwasi
akawaambia
wamueleze
watakapompata
Yesu.



"Pia nami nataka
kumwuabudu."
Herodi
akawaambia.
Lakini alikuwa
anawadanganya.
Herodi
alitaka
kumwua
Yesu.





Ile nyota ikawaongoza hadi horini
Maria na Yusufu
walimokaa na
mtoto Yesu.





Wakipiga magoti wakimwuabudu,
wale wasafiri walimpa
Yesu zawadi za
kupendeza za
dhahabu
na manukato.





Mungu akawapa wale
wazee hadhari
kuwa warudi
nyumbani kisiri.





Herodi alikasirika
sana alipogundua
haya.



Kwa hamu ya
kumwuangamiza
Yesu, ...



... kiongozi huyu
mwovu aliwaua
watoto wote
wachanga wa kiume
kule



Bethlehemu.



Lakini Herodi
hangeweza
kumwamgamiza
mwana wa
Mungu!






Walipohadhariwa
kwa ndoto,
Yusufu
aliwachukua
Maria na Yesu
penye usalama

kule Misri.





Herodi
alipoaga dunia, Yusufu
akawatoa Maria na Yesu Misri.





Wakaishi katika
mji mdogo wa Nazareti
iliyokuwa karibu na ziwa la Galili.



Kuzaliwa kwake Yesu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu,
Bibilia,

inapatikana katika

Matayo 1-2, Luka 1-2

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu
Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na
anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya,
anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni
mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata
akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili
afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi
yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda
nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na
kumwomba msamaha kwa dhambi yako,
Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani
yako, na utaishi naye milele.



Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya
kwa Mungu:

Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni
Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya
dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na
siku moja nitaenda kuwa nawe millele.
Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama
mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila
siku! Yohana 3:16

